

KIDATO CHA KWANZA
KISWAHILI
MUHULA WA KWANZA 2016
MUDA:

JINA:.....NAMBARI YA USAJILI:.....

DARASA:TAREHE:.....

MADA	ALAMA	
UFAHAMU	15	
SARUFI	40	
FASIHI SIMULIZI	10	

UFAHAMU

Yamesemwa mengi kuhusu ufisadi. Si wanasiasa si mapadiri, si mashehe, si viongozi wengineo wa jamii, wote wametoa mchango wao juu ya suala hili nyeti. Kila linaloenda kombo, sababuye, ufisadi. Nchi haina maendeleo kiini – ufisadi. Kusambaratika kwa miundo msingi asili yake ufisadi.

Je, hapo ulipo wewe unauielewa ufisadi kuwa ni nini? Je, umewahi kujituliza na kutafakari juu ya ufisadi? Unahusika vipi na ufisadi? Umewahi kuathirika na ufisadi, wewe binafsi au kupitia kwa aila na masahibu? Kila mmoja aliye mzalendo halisi anapaswa kujisaili nafsi yake kupitia kwa maswali haya.

Wakati ukiendelea kuzingatia maswali haya hebu tuzame kwenye kina cha ufisadi. Kijelezi cha ufisadi; ni ile hali ya kutenda au kushiriki matendo yanayosababisha uharibifu au uborongaji wa kanuni au taratibu zilizokubalika kutekelezea mambo. Katika hali hii ufujaji na ubanangaji huwa vyombo vya ufisadi. Madhumuni yake ya jumla ni kubatilisha haki, kuvutana na haki na hatimaye kuifanya isifuata mkondo wake sahihi.

Kwa kuwa jambo halizuki kighaffa tu, tunapaswa kujiuliza maswali haya: Waasisi wa ufisadi hupata motisha wapi? Huukuza kwa azma gani? Kimsingi, chimbuko la ufisadi ni ubinafsi uliozidi. Mbegu ya ufisadi ni uchoyo, huchipuza uchoyo na kukomaza uchoyo. Mizizi shina, matawi, majani na hata matunda yake ni uchoyo uliokithiri. Dhana ya kujiwazia kibinafsi katika shughuli zote ndiyo huupa ufisadi nishati ya kujiendeleza. Kila mja ana kiwango fulani cha ubinafsi. Hali hii ndiyo hupelekea kujitahidi kwa jino na ukucha ili kujihifadhi na kujiendeleza. Ubinafsi wa aina hii si mbaya kwani humpa binadamu msukumo wa kujishughulikia kwa lengo la kujipatia natija inayofaidi aila, jamii na hatimaye taifa kwa jumla.

Uchoyo wa *mimi-hiki, mimi-hicho, mimi-kile* na hatimaye *mimi-kila kitu* ni uchuro. Ufisadi nao ni uchuro. Ni dude, jinyama, jipweza lenye minyiri isiyohesabika. Minyiri hiyo imepenya katika nyanja zote za maisha, ya mtu binafsi hata ya taifa kwa jumla. Ufisadi umeshamiri na kuzagaa hadi kufikia kiwango cha kimataifa.

Tukirejelea suala la awali kabisa itadhihirika kuna ufisadi katika mambo ya uvyazi. Vuta taswira hii ya waja wazito wawili ambao siku zao zimewadia. Mmoja anajiweza, anawasilishwa hospitalini kwa gari. Wa pili hana nyuma wala mbele amefika kwa miguu au pengine kwa rukwama. Kisia mwenyewe ni nani atakayehudumiwa kwanza. Ukitafti utagundua sababu ni ufisadi. Mmoja atatadarukiwa ilhali wa pili atakawilishwa. Haya pengine ni kutokana na matumaini ya kupewa bakshishi ambayo kwa kweli ni namna ya hongo. Kumbuka, wahudumu wawa hawa ni waajiriwa wapokeao mishahara mwisho wa mwezi.

Mambo ni yayo hayo kitokeapo kifo. Ndugu, jamaa au rafiki anapoaga dunia huenda ukajikuta matatani. Licha ya majonzi yanayoambatana na mauko, utasombeshwa mzigo wa kuwarairai wahudumu wa ufuo ili ushughulikiwe. Wanajua hali uliomo na hapo tena matumaini ya kadhongo yatajitokeza. Na iitwe bakshishi si hoja. Huu ni ufisadi. Haki na linalopasa ni kuipata hiyo huduma kwa gharama rasmi bila haja ya bakshishi ambayo si bakshishi bali rushwa.

Naam, ufisadi tunao kati yetu, katika shughuli za kila aina. Fikiria juu ya wapanga foleni mahali fulani wanaongojea kuhudumiwa. Wewe ufike wa mwisho, umwite mhudumu maana mnajuana, uhudumiwe sawia. Ni ufisadi! Umesababisha utanguaji wa utaratibu

sahihi uliokuwapo. Athari zake ni kuwa waliorauka hawakushughulikiwa kwa wakati wakacheleweshewa yao. Wewe nawe unaajizika kwa kuzoea kupendelewa.

Katika amali za biashara uborongaji wa taratibu unadhihirika hasa katika utoaji wa zabuni za miradi mbalimbali ambapo suala kubwa ni kasma. Kiasi na jinsi ni baada ya kuhakikisha kuwa tenda imeliendea shirika fulani. Kasma lazima ipatikane! Si hoja kuwa pesa za kugharamia miradi hii zimetokana na ruzuku au mikopo kutoka kwa wafadhili. Ghushi za kila aina zitatumiwa ili kasma ipatikane. Katika hali kama hii si ajabu matokeo ni kuharibika kwa miundo msingi katika sekta mbalimbali zinazohusika na usambazaji wa huduma kwa wananchi.

Kwingineko ukiukaji wa taratibu za ulipaji na ukusanyaji wa ushuru kumeupa ufisadi mboji ya kuotesha mizizi yake. Wako wafanyibiashara watakatua 'kitu kidogo' ili kufikia hali ya ukiritimba ilhali washindani wao wanakwazwa kwa kutozwa kila aina ya ushuru. Sekta ya kilimo nayo haikuepuka athari hizi za kubananga na kukiuka maadili. Hali ya wachache kupewa nafasi ya kuagizia bidhaa bila kulipia ushuru na ambazo zinazalishwa humu nchini imejikita katika uchoyo. Bei za bidhaa kama hizo bila shaka zitakuwa nafuu kuliko za humu nchini. Kwa upande mwingine, mkulima anatarajiwa kufanya nini na rundo la mazao yasiyo na soko? Msururu wa matatizo ukianzia hapo hauwi na kikomo.

Ni dhahiri shahiri kuwa kila mmoja anapaswa kujumuika katika kitali hiki dhidi ya ubinafsi, ufisadi na ubanangaji. Wote tukianzia na viongozi tunapaswa kujifunga nira kupambana na ufisadi. Wananchi wahamasishwe juu ya wajibu wao katika vita hivi vikali. Wote tuzinduke na kufahamu hicho kidogo cha ziada, hiyo fadhili, hayo mapendeleo ambayo msingi wake ni kuvuruga utaratibu yatatuponza. Changamoto kwa kila mmoja wetu ni: Tuko tayari kuziasa nafsi zetu ili zitambue athari za ubinafsi na hivyo kuzikabili vilivyo?

Tutakapotambua kuwa waendelezaji wa ufisadi ni **MIMI** na **WEWE**, hapo ndipo vita dhidi yake vitaanza kufanikiwa.

1. Ipe taarifa hii kichwa mwafaka. (al 1)

.....
.....

2. Eleza maana ya ufisadi. (al 2)

.....
.....
.....

3. Eleza chimbuko la ufisadi. (al 2)

.....
.....
.....
.....
.....

4. Kwa nini mwandishi anafananisha ufisadi na uchuro, jinyama au jipweza? (al 2)

.....
.....
.....
.....

5. Taja maneno ambayo ufisadi hutekelezwa. (al 5)

.....
.....
.....
.....
.....
.....

6. Eleza njia moja ya kukomesha ufisadi. (al 2)

.....
.....

7. Taja maneno mawili yenye maana sawa na ufisadi. (al 1)

.....
.....

SAFURI (ALAMA 40)

Maagizo: Jibu maswali yote.

(a) Lugha ni nini? (al 2)

.....
.....

(b) Eleza sifa mbili za lugha. (al 2)

.....
.....
.....

(c) Fafanua umuhimu wa lugha. (al 2)

.....
.....
.....
.....

(d) Eleza tofauti kati ya irabu na konsonanti. (al 2)

.....
.....
.....

(e) Tofautisha sauti zifuatazo. (al 2)

(i) /a/ na /o/.....
.....
.....

(ii) /j/ na /k/
.....
.....
.....

(f) Taja vikwamizo viwili vya midomo meno. (al 2)

.....
.....

(g) Unda maneno kutokana na muundo wa silabi zifuatazo. (al 2)

K I.....
K K I.....

(h) Ainisha vipashio vya lugha huku ukitoa mifano. (al 2)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

(i) Kiambishi ni nini? (al 2)

.....
.....
.....

(j) Ainisha viambishi awali na tamati katika vitenzi vifuatavyo. (al 2)

(i) Tuliempiga
.....
.....

(ii) Ulivyoniletea.....
.....
.....

(k) Bainisha viambishi katika maneno yafuatayo. (al 3)

Waliyempiga
.....
.....
.....
.....
.....

(l) Tofautisha kiimbo na shadda. (al 2)

.....
.....
.....
.....
.....

(m) Bainsiha matumizi mawili ya kiimbo. (al 2)

.....
.....
.....
.....

(n) Tofautisha maneno yafuatayo kwa kutia shadda. (al 2)

(i) Ala.....
A la.....
(ii) Walakini.....
Walakini.....

(o) Tia shadda katika sentensi zifuatazo. (al 2)

(i) Kitabu cha mwanafunzi ki mezani.
(ii) Wanafunzi wamo darasani.

(p) Tofautisha sentensi zifuatazo kwa kutia shadda. (al 1)

Wacheza kandanda.

Wacheza kandanda.

.....
.....

(q) Akifisha sentensi ifuatayo. (al 2)

wageni kutoka afrika kusini walikaribishwa na rais moi.

.....
.....
.....

(r) Tunga sentensi kuonyesha tofauti ya vitate hivi. (al 2)

Papa

Baba

.....
.....

(s) Tunga sentensi katika wakati timilifu katika nafsi ya kwanza umoja. (al 2)

.....
.....

(t) Nyambua vitenzi vifuatavyo. (al 2)

Kitenzi	Kutendea	Kutendewa
Piga		
Lima		

(u) Kamilisha methali ifuatayo. (al 1)

Akumegeaye tonge...

.....
.....
.....

FASIHI SIMULIZI (ALAMA 10)

1. Fasihi ni nini? (al 2)

.....
.....
.....

2. Taja makundi mawili ya fasihi simulizi? (al 2)

.....
.....
.....

3. Eleza tofauti zozote tatu za Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi. (al 6)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....